Global Fund for Community Foundations

Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii

Zaidi ya kitu chenye mwanzo hafifu?

Kuibuka kwa taasisi jamii kama dhana mpya ya Maendeleo

Jenny Hodgson na Barry Knight

Jenny Hodgson ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii

Barry Knight ni Mkurugenzi Mtendaji wa CENTRIS na Mshauri wa Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii.

Katika kuandaa makala hii, mwandishi alichukua zaidi mahojiano yaliyofanywa na Andrew Milner (CENTIRIS) na Vadim Samorodov (Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii) na wapokea ruzuku wa Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii. Avila Kilmurray, Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi Jamii wa Ireland ya Kaskazini na mjumbe wa bodi ya Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii, alisaidia kutafsiri matokeo ya utafiti.

Makala hii imetafsriwa na: Elikira Kweka
IRTECO-Tanzania,
Baruapepe: elkweka@yahoo.com
September 2010

Yaliyomo

Utangulizi	2
Muhtasari	3
Vyanzo vya takwimu	4
Kutafsiri eneo	4
Changa na ndogo	5
Ukubwa sio kila kitu; ni shughuli ndizo zinazohusika	7
Kujenga jamii kakamavu	7
Kushirikisha jamii	9
Taasisi ya jamii na haki ya jamii	10
Ruzuku ndogo ndogo kama zana ya maendeleo	11
Utoaji wa fedha na ukusanyaji wa fedha	12
Hitimisho	15
Nini kingine	15

Utangulizi

Makala hii inaanza kuleta matokeo kutoka utafiti wa takwimu za msingi za maombi 50 ya msaada kutoka Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii. Makala imetumia taarifa zilizopatikana kutokana na michakato ya kutathmini ruzuku ili kupata uelewa juu ya hali halisi katika eneo hili, inaweza kuchangia nini dhidi ya mapato na athari, na nadharia tete katika kuendeleza kazi ya namna hii.

Makala inapendekeza kwamba hisani kwa jamii ambazo ni maskini inaweza kuwa na nafasi muhimu katika kutengeneza enzi mpya ya maendeleo. Makala hii imejikita katika kikundi cha wapata ruzuku ambacho kitafuatiliwa kama sehemu ya kazi ya tathmini na Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii.

Muhtasari

Hisani kwa jamii zenye umaskini kwa muda mrefu imekuwa ikichukuliwa kama 'kitu chenye mwanzo hafifu'katika ulimwengu mpana wa hisani. Lakini hii inahitaji kubadilika. Taarifa yetu inasema kwamba hisani kwa jamii maskini na taasisi jamii, mbali ya kuwa pembezoni, sasa zinajitokeza kama sehemu za kuendeleza katika eneo pana la maendeleo ya mataifa.

Imekuwa ikipendekezwa kwa muda mrefu kwamba jamii ziwe zinashirikishwa kiundani zaidi katika maendeleo yao wenyewe. Mtizamo huu ulijitokeza miaka ya 1940 wakati tawala za kikoloni zilipoanza kupanga kuhamishia mamlaka kwa dola zilizojitokeza, na kupata maelezo kamili miaka ya 1960 wakati wa 'vita vya umaskini' Marekani, wakati gumzo lilikuwa 'uwezekano wa ushirikishwaji mkubwa.' Nadharia ilikuwa kwamba wenyeji walihitaji kumiliki mipango ya maendeleo na kujenga kuaminika katika taasisi ambazo zilitoa msaada; vinginevyo 'ukiritimba baridi' ungetawala maendeleo.

Bahati mbaya, wazo la 'jamii' limekuwa likitegemea mabadiliko ya mitindo katika kutekeleza maendeleo na daima haijachukua njia imara. Hii kwa sehemu moja ni kwa sababu ni wazo gumu kutekeleza, na ukosefu wa uelewa juu ya misamiati iliyotumika, ugumu wa kupata taasisi za jamii madhubuti kutoa mpango,na uelewa hafifu wa namna ya kupima athari. Kwa sababu hizi, kila mmoja huunga mkono wazo la 'jamii' lakini kwa ujumla hakuna hata mmoja anayetenda. Hata hivyo,bila ushirikishwaji wa jamii, ushahidi ni kwamba mipango ya kutoka juu hushindwa kutoa faida ya mwisho.

Waraka huu unalenga kuandika matokeo muhimu ya maendeleo – matokeo ya zaidi ya miaka 15 ya taasisi jamii katika kipato kidogo na cha kati cha namna tofauti kutoka Kusini ya Dunia – kutoka Brazil hadi Thailand na kutoka Afrika Kusini hadi Azerbaijani. Ushahidi uliokusanywa kutoka taasisi hizi –unakiri kundi dogo-hulenga umuhimu wa ukuaji wa maendeleo ya jamii yanayo-tengenezwa katika hali halisi. Hii huonyesha mikakati ya kuhama kutoka juu kwenda chini ya serikali nyingi na mipango ya kimataifa ya misaada kwenda 'maendeleo yanayosimamiwa na watu wenyewe.'



Ukuaji wa taasisi za kijamii kote duniani umeonyeshwa katika chati 'Ukuaji katika taasisi za kijamii.' Uchambuzi wa mwelekeo unaonyesha kwamba ukuaji ni thabiti na kwamba,kwa wastani, taasisi za kijamii 70 zinaundwa kila mwaka.[2] Idadi jumla imeongezeka zaidi ya mara mbili kidunia ndani ya miaka kumi.

Eneo la taasisi jamii katika Kusini mwa Dunia na katika chumi zinazojitokeza za Mashariki ya Ulaya bado ni changa na ndogo kifedha. Hata hivyo, utafiti huu unapendekeza kwamba hii sekta inayojitokeza inatoa utambuzi wenye nguvu katika kuongeza uaminifu wa jamii, kutia moyo ushiriki wa wenyeji, kutatua masuala ya sheria za jamii, na kuongeza majukumu ya mali za jamii. Kama michakato hii ingefanyika kwa mpangilio, hii ingeweza kutokea kwa enzi mpya kwa maendeleo ya kimataifa.

Vyanzo vya takwimu

Taarifa hii inatolewa katika vyanzo vikuu vitatu vya ushahidi:

1. Uzoefu wa miaka mine wa Mfuko wa Dunia wa Taasisi za Jamii wa kuunda misaada midogo midogo (Dola za kimarekani 5000 hadi 50,000) kwa taasisi za jamii 121, waundaji misaada wengine wa ndani, mashirika ya hisani na jumuiya katika nchi 41 kuzunguka Latini Amerika,Afrika,Mashariki ya Kati,Asia na Ulaya Mashariki;
2. Matokeo ya muhtasari muhimu ya tathmini ziliyofanyika kuhusu Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii kwa kutengeneza misaada kutoka 2006–08;
3. Takwimu za muda na za kisayansi zilizochukuliwa kutoka mikakati mipya kwa ukusanyaji takwimu ambapo Mfuko wa Dunia waTaasisi Jamii ulijaribu wakati wa mzunguko wa ruzuku yake mwaka 2009. Takwimu za msingi za 'watu' zilikusanywa kutoka fomu za maombi kwenye taasisi za jamii 49 na mashirika ya misaada ambayo yalikaribishwa kuwasilisha maombi kamili.[3] Maombi pia yalikaribishwa kufikiria matokeo ya kazi yao kwa kuoanisha vipaumbele kupitia viashiria tofauti vilivyojengwa na Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii. Hii ilifuatiwa na mahojiano ya kina na mashirika 37 (ikishirikisha wote waliofanikiwa kusaidiwa pamoja na mashirika ambayo maombi yalikataliwa).

Tunafahamu kwamba, kuhusiana na eneo pana la hisani za jamii, takwimu zinapendelea kuelekea mashirika madogo na yaliyo kusini. Hata hivyo, makala hii ni hatua ya mwanzo katika bidii pana ambayo tayari imepangwa na sisi kupata takwimu kwa mpangilio zaidi juu ya eneo hili. Ingawa takwimu ni za muda, pia ni ufafanuzi wa mwelekeo unaofanyika ndani ya eneo, zaidi hasa Kusini mwa Dunia.

Kutafsiri eneo

Kwa upana, mashirika yaliyopitiwa katika waraka huu yanaangukia katika makundi makuu manne:

1. Taasisi Jamii: ilianzishwa (wakati mwingine na msaada wa kimataifa na wakati mwingine bila) kwa makusudi ya marejeo kwa baadhi ya 'kanuni' za taasisi za dunia za jamii na kawaida kukubalika katika mazingira ya eneo;
2. Asili, mara nyingi kitaifa,taasisi za kutoa ruzuku:anzishwa kwa ukubwa na mfuko wa kimataifa na ambao unatafuta kuendeleza hisani ya ndani kama mikakati ya uendelevu wa muda mrefu na pia kuendeleza haki yao ya eneo na umiliki;
3. Moyo wa kujituma ambao unaweza kuelezwa kama 'kufanana na taasisi ya jamii' kiasili: zina tabia zinazofanana na thamani kwa taasisi ya jamii,ambayo inatafuta

aidha kujijenga juu ya utamaduni uliopo wa uongozi na hisani au shughuli zilizopo kupitia 'lenzi' za taasisi ya jamii;

4 Namba ndogo (7) ya mashirika ya hisani (kwaida uanachama wa jumuiya), juhudi katika maendeleo ya taasisi jamii katika nchi maalum au eneo.

Kundi limegwanyika sana katika umri, ukubwa na mazingira ya ndani. Licha ya huu mchanganyiko, mashirika yote yaligawana muunganiko wa namna moja ya kundi la shughuli za msingi, ambazo zilihusisha utoaji wa ruzuku, maendeleo ya hisani za ndani, na masuala magumu ya majukumu ya 'kujenga njia ya kuunganisha' jamii chini ya paa la taasisi moja.

Eneo

Mgawanyo wa wapokea ruzuku kwa eneo umeonyeshwa katika chati ifuatayo.

Sehemu ya wapokeaji



Changa na Ndogo

Taasisi jamii zilizopitiwa katika utafiti huu zote zilianzishwa baada ya 1992, umri wa kati ulikuwa miaka minne,na tatu – tano kati yake zilikuwa na miaka mitano au chini.[4] Taasisi ziliulizwa kusema ni vipi waliona hatua yao ya maendeleo. Matokeo yameonyeshwa kwenye chati. Ni wazi kutoka kwenye chati kwamba taasisi zilijiona zenyewe katika hatua ya mwanzo ya maendeleo.

Namna mashirika yaonavyo hatua yake ya maendeleo



Zaidi ya kuwa changa, taasisi hizi za jamii kwa kiasi pia zilikuwa siyo kubwa sana katika masuala ya fedha. Ukiacha mashirika machache yenye pato la mwaka ambalo lilizidi dola za Kimarekani 750,000–dola milioni 1, robo tatu walipokea chini ya dola 155,000 katika pato, na nusu chini ya dola 65,000. Robo moja walikuwa na mapato chini ya dola 23,000.

Kulikuwa na mahusiano ya kitakwimu kati ya urefu wa muda shirika limekuwepo na kiwango chake cha pato lakini madhara ya umri kwenye pato haikuwa sababu kubwa.

Hii inaweza kuonekana katika mchoro mtawanyo ufuatao. Kila nukta inawakilisha taasisi,ikionyeshwa kwa umri katika mhimili mmoja na pato mwaka 2009 kwa mhimili mwingine.

Mwelekeo kwa ujumla umeonyeshwa kwa mstari mweusi, ambao unaonyesha ongezeko la pole pole na kwa kipindi kirefu. Hata hivyo, hii nyongeza kidogo kidogo inaficha mabadiliko makubwa naya haraka – na mstari wa bluu ulioiva unaonyesha tukio kubwa, mstari mwekundu tukio juu ya wastani na mstari kijani hafifu unaonyesha kundi la mashirika ambayo yalipata pato dogo katika kipindi.

Umri na pato



Ukubwa sio kila kitu; shughuli ndiyo hoja

Tumekuta kwamba ukubwa wa taasisi jamii ulikuwa na umuhimu mdogo kuliko majukumu inayotekeleza katika jamii. Tuliuliza watu kutathmini majukumu waliyotekeleza, kutoa kwa vipi ilikuwa muhimu[4]. Matokeo yanaonyeshwa katika chati ifuatayo. Alama ni makadirio ya wastani katika mizania ya alama – tano ambapo 1 ni 'chini sana' na tano ni 'juu sana'.

Umuhimu wa shughuli mbalimbali



Inafaa kuzingatiwa kwamba vitu vyote katika robo ya alama za juu (zote zenye kiwango cha 4 au zaidi) inashirikisha neno 'jamii', ambapo hata moja ya zilizo katika robo ya chini (alama ya 3.25 au chini) inafanya hivyo. Ni wazi kwamba kazi za msingi kwa taasisi katika jamii hii inaangalia mambo kama kujenga uaminifu, mshikamano, mali na uwezo ndani ya jamii.

Matokeo haya yalithibitishwa katika mahojiano na mashirika. Ingawa utengenezaji wa hisani ulikuwa ni kazi ya msingi kwa takriban mashirika yote yaliyohojiwa – na moja ambalo lilijaribu kutofautisha wao kutoka mashirika mengine ya kijami katika jumuiya yao – wengi waliona jukumu lao la msingi kama kukuza mali za jumuiya yao.

Kujenga jamii amilifu

La msingi na jukumu la taasisi ya jamii ilikuwa kujenga mahusiano kati ya sehemu mbalmbali za jamii, kuendeleza uaminifu kwa jamii na kuamsha utamaduni wa hisani za ndani. Katika kutekeleza majukumu haya,wahojiwa wanaofanya katika taasisi jamii

waliona kazi zao kuwa kama juu ya kutia watu moyo kuwa waamilifu zaidi katika maendeleo yao wenyewe, ikiongozwa na mawazo kwamba 'watu wanaweza kufanya mambo wao wenyewe'. Pia walizungumza jinsi walivyojaribu kushinda viwango vikubwa vya kutokupenda kubadilika na kutojihusisha na uraia katika jamii zao kwa 'kufanya watu kuchukua usimamizi wa maisha yao', kama mmoja alivyoliweka.

Kwa kusisitiza jukumu la uchangiaji wa ndani kama raslimali ya ndani ya jamii kuweza kuanzisha jambo, taasisi za jamii mara kwa mara walijikuta wenyewe wakipinga jinsi wenyeji wanavyofikiri na kuamua mambo kwa tofauti kubwa kabisa,hasa katika kuondoa uono wa jamii kama wapokeaji mara zote. Hii ilikuwa hasa katika hali katika mazingira ambapo msaada wa kimataifa ulitengeneza utamaduni wa utegemezi, pamoja na katika nchi za mwanzo za kundi la Mashariki ambapo dola kwa desturi zilifanya usimamizi toka juu kwenda chini. Wengine walihimiza wasaidiwaji kuanzisha mfuko wa matembezi kama namna ya kuongeza umiliki wa ndani na wazo la kujitegemea – au, kwa maneno ya mtoa majibu mmoja, 'kubadilisha namna wanavyoona wenyewe na kila mwingine'.

Taasisi nyingi pia ziliona jukumu muhimu katika kuonyesha kwamba taasisi makini zingeweza kuimarisha mahusiano ya jamii na bidii za maendeleo ya ndani. Katika mazingira ambayo uaminifu kwa umma ulikuwa haupo au umemomonyolewa na rushwa, hii ilikuwa kama zaidi juu ya kurudisha imani katika taasisi. Katika hali nyingine, mashirika yalikuwa yanatafiti namna ambayo muundo wa taasisi mpya ungeweza kuingizwa na kuundwa kuunga mkono tamaduni za asili. Shirika moja lilofanya kazi na jamii ya asili katika Latini Amerika lilikuwa linatafuta kuingiza taasisi ya jamii kama namna ya kuongeza ufahamu wa thamani ya muundo wa taasisi na jamii zake. Katika mfano mwingine katika Asia ya Kati, muundo wa kitaasisi wa taasisi jamii ulikuwa umeanzishwa kama nyenzo sahihi ya utawala ndani ya muundo wa kiasili wa utawala na utamaduni wa kusaidia.

Nyingi ya taasisi za jamii zilikazia umuhimu wa majukumu yao kama wafadhili wa ndani wa kujitegemea wa ndani, huru kutokana na ushawishi wa mfadhili yeyote au kundi lenye nia. Hayo maono ya uhuru pia yalitajwa na wengi ambao waliojiona wenyewe kama wanatekeleza jukumu maalum katika kuunganisha na kukutanisha makundi mbalimbali ya jamii. Wengi wanafafanua namna jukumu hili kama 'mwezeshaji wa jamii' haikuwa lazima moja ambayo mwanzoni ilitafutwa kwa bidii, lakini badala yake ilikuja kwao walivyokuwa wameanza kujenga majimbo yao ya asili kama watengenezaji wa ruzuku na wachangishaji wa mfuko wa ndani. Ruzuku ndogo kwa sehemu mbalimbali za jamii ziliziwezesha taasisi za jamii kujenga mahusiano ya uaminifu na mashirika ya ndani na makundi na kujenga msingi wa maarifa wa mahitaji ya ndani pamoja na uwezo wa makundi ya ndani. Hii-pamoja na mafanikio na uwazi wa usimamizi wa ruzuku-pia iliongeza heshima yao kwa sehemu zingine za jamii (ikiwemo serikali, wafadhili wa ndani na umma kwa ujumla) na kuimarisha nafasi yao kama 'mjenzi wa daraja la asili'. Mmoja alifafanua taasisi jamii yao kama 'shirika ambalo watu wanakuja'. Taasisi jamii changa Kusini Mashariki mwa Asia ilisema 'tunafahamika kama wakutanishaji wa matatizo magumu'.

Kushirikisha jamii

'Jamii kushiriki kulionekana kuwa muhimu kwa kazi za taasisi zote zilizochunguzwa. Katika maneno ya shirika moja, 'Huwezi kuwa taasisi ya jamii kama jamii haijishughulishi na wewe'. Hata hivyo, uunganishaji wa maeneo yanayojitokeza na ueneaji mdogo wa taasisi jamii ilimaanisha kwamba uhamasishaji wa umma ulikuwa mdogo,na mashirika mengi yalielezea namna ilivyokuwa ngumu wenyewe kujieleza kwa jamii.

Dhana kama 'hisani' ingeweza kuwa ngumu kukubalika,hasa kulipokuwa na historia ya kutokuaminika kwa neno (kama katika nchi za zamani za kijamaa ambapo iliambatana na michango ya hiari kwa mujibu au 'kujitolea kwa mujibu') au katika mazingira ambapo desturi ya kutoa na kusaidiana pamoja (kama jumuiya ya kuzikana na uokoaji 'mambo yanayotokea ghafla') ulitengeneza mfumo muhimu wa kijamii wa kusaidia matatizo makubwa katika jamii maskini na bado kwa ujumla haikufikiriwa kama mfuko wa 'maendeleo'. Kitendo cha kutengeneza misaada pia mara nyingi kilichukuliwa kama kitu kipya na kawaida zaidi kuambatana na mipango mikubwa ya mashirika yasiyokuwa ya kiserikali.

Licha ya vikwazo hivi,karibu kila (asilimia 96) taasisi ya jamii imetumia mikakati tofauti yenye lengo la kuendeleza aina mbalimbali za ushiriki, ikihusisha mikakati ya kufanya kutokea utengenezwaji ruzuku kufikia makundi yasiyo rasmi au makundi yaliyo pembezoni,uchangiaji ruzuku kwa umma au matukio ya kujitolea na ushiriki katika mbinu za kufanya maamuzi katika taasisi jamii (ikiwemo kamati za ruzuku n.k). Mikakati mingine iliyotumiwa na taasisi jamii kusikiliza kwa, kujifunza kutoka na kujenga kujiamini katika jamii zao ikiwemo vikao vya mashirika yasiyo ya kiserikali, benki za vijana, mashauriano na jamii,mikutano ngazi za vijiji na mfumo wa jamii wa ufuatiliaji. Katika hali kadhaa,dhana ya 'jamii' yenyewe ilikuwa ni wazo lililoshindana: hii hasa ilikuwa hali kwa taasisi jamii ambao majimbo yao makuu yalikuwa watu ambao walikuwa wanawekwa pembeni na 'jamii' kubwa. Pia ilijitokeza kama suala katika mazingira mengine ambapo misukumo ya kiuchumi au kijamii wakati mwingine ilipelekea kupunguzwa kwa tafsiri ya jamii.

Wote waliopitiwa walisisitiza umuhimu wa ushiriki wa jamii katika sura tofauti ya kazi zao. Hata hivyo, hii mara zote haikutafsiri katika muundo wao wa utawala. Asilimia 57 tu walikuwa na mchakato wa wazi wa uchaguzi kwa wajumbe wa bodi na asilimia 50 walikuwa na vipindi vya kudumu vya ujumbe wa bodi. Moja ya maelezo ya dhahiri ya udhaifu katika eneo hili ni kwamba mengi ya mashirika katika kundi yalikuwa bado tu yanaanzishwa.

Wakati muhimu na hatarishi wa kuanza awamu,wakati ambapo taasisi jamii ilitangaza uwezo wake,msaada kwa bodi ndogo, iliyochaguliwa kwa uangalifu yenye watu wa heshima – mara nyingi kutoka ndani ya mwendelezo wa mtandao wa waanzilishi-ambao kwa upana wanaelewa wazo na kutoa kibali kwa taasisi,ilikuwa muhimu.

Ili mradi taasisi jamii ilikuwa inajishughulisha na jamii katika masuala mengine ya uendeshaji wake, bodi iliyochaguliwa kimkakati ingeweza kusaidia na kulinda nafasi ambayo shirika lilikuwa linatafuta kujiweka lenyewe wakati linajenga uelewa na kukubalika ndani ya jamii kubwa. Mashirika mengi yenye bodi iliyochaguliwa kwa umakini wakati wa kuanza awamu walikuwa wanajiandaa kwa mpito kwenda bodi ambayo ilikuwa imemizaniwa zaidi na kuwakilisha jamii pana.

Katika suala la bodi, inafaa kuzingatiwa kwamba kulikuwa na namna nyingi ambapo taasisi jamii ilikuwa imeanzishwa kupitia hatua ya aina fulani ya uwezeshaji wa nje. – mara nyingi kwa msaada wa mfuko wa kimataifa – na ambapo miundo ya

utawala ilijaribu kuwa zaidi na mpangilio rasmi lakini ambapo taasisi jamii bado ilikuwa inakazana kutafuta mwelekeo wake kwa sababu ya mchanganyiko wa uzoefu mbalimbali na uelewa ndani ya nadharia yake ya wawakilishi wa bodi.

Taasisi ya jamii na haki ya jamii

Takwimu zetu zinaonyesha kwamba taasisi jamii zinajenga mtaji jamii katika jamii inazohudumia – mfululizo wa mawazo ya kawaida ya kuendeleza ushiriki wa wananchi na kuongeza imani ya mwanachi kuonekana kuwa thabiti.

Upitiaji wetu pia ulichunguza kiasi ambacho taasisi jamii ilichukua katika muundo au masuala magumu ya haki jamii. Tuliuliza maswali kuhusu jinsi wasaidiwaji walivyoelewa maana ya 'haki jamii',iwapo lilikuwa neno katika matumizi ya kawaida, iwapo ilikuwa na maana nyingine ya zaidi kwa bahati mbaya,na kama hivyo walitumia mbadala gani. Tulitumia pia mbinu zilizotengenezwa na Kikundi Kazi katika hisani kwa Haki Jamii na Usalama.[5] Kikosi kazi kilipendekeza kwamba 'haki jamii'ni wazo la jumla sana kuwa na maana isipokuwa likichambuliwa katika desturi maalum ya fikra kama 'haki za binadamu' au 'ugeuzaji wa muundo'.[6] Kutokana na hili, uchambuzi tulipata kauli maalum sita kwa haki jamii (bila kutumia hiyo alama) na kuuliza ni kwa kiasi gani zililingana na matokeo ya kazi ya taasisi katika skeli ya alama-tano.

Ilikuwa wazi kwamba kwa asilimia 17.6 ya waliohojiwa,msemo 'haki jamii'ulibeba aina fulani ya maana nyingine zaidi kwa bahati mbaya na tafsiri iliyofanya matumizi yake kuwa tatizo. Hii ilikuwa hivyo hasa katika mazingira ya Ujamaa uliopita ambapo uliambatana na itikadi za kikomunisti ambazo zilipendekeza wazo la jamii (umiliki was serikali) dhidi ya mtu binafsi. Wakati huo huo,hata kule ambapo 'haki jamii'haikubeba dalili hasi za hisia, sehemu kubwa ya watu (asilimia 58.8) walipendelea kutumia neno lingine. Wakati watoa majibu wengi walisikia faraja kuelewa na kutumia neno ndani ya mizunguko fulani (taasisi jamii mwenza na mitandao,wachangia mifuko wa kimataifa n.k), wengi waliona kwamba ingeweza kuwa jumla zaidi kutumika kwa manufaa kwenye mahitaji ya haraka au kwamba kulikuwa na hatari ya matumizi yake kusababisha uwezekano wa kutokukubaliana kwingi baina ya watu au siasa za wazi miongoni mwa sehemu tofauti za jamii. Mdodoswaji mmoja alijumuisha hii kama:

> 'Hatutumii neno 'haki jamii'moja kwa moja, lakini ni kanuni muhimu katika kazi yetu. Watu wangeunganisha neno hili na siasa ambayo haina manufaa sana katika nchi yetu na lazima tuwe makini na kuwa wapinzani'.

Ijapokuwa na wasiwasi juu ya lugha, wakati ilipokuja katika suala la kazi kwenye haki jamii, watu kawaida walitoa alama kubwa kwenye tamko sita zilizopatikana kutoka katika kazi ya Kikundi Kazi cha Hisani kwa Haki Jamii na Usalama. Hizi zimeonyeshwa katika jedwali lifuatalo. Alama ziko katika skeli ya 1 hadi 5 (ambapo 1 ni chini na 5 ni juu)

Kigezo cha haki jamii	*Wastani*	*Muachano wastani*
Muundo ambao unahakikisha mgawanyo sawa wa matokeo bidhaa za umma na binafsi	3.58	1.23
Watu wote wana ulinzi ndani ya mfumo wa haki	3.71	1.35
Makundi ya pembezoni yanalindwa kupitia utawala wa sheria	3.74	1.21
Watu binafsi na makundi wana nguvu kuwa na usemi kwenye mambo ambayo yanawagusa wao	4.39	0.88
Tamaduni zote zinatambua kwamba kanuni zao hazimiliki wengine	3.58	1.2
Soko linajiendesha katika namna ambayo hufaidisha wote	3.48	0.89

Inavutia kwamba alama ya juu ni 'watu binafsi na makundi yenye nguvu ya kuwa na msemo kwenye mambo ambayo yanawagusa'. Hii inaungana na matokeo yetu ya awali juu ya kuongeza nguvu ya jamii.

Inafaa kuzingatiwa kwamba alama ya juu kwenye moja ya vigezo sita inabashiri alama ya juu kwa vyote vilivyosalia.[7] Hii ina maana kwamba kuna kisababishi dhahiri cha wazo kuunga mkono hivi vitu sita-ambapo watu wanaweza kuita haki jamii au kitu kingine, lakini huonekana kuwa sawia na mawazo ya haki jamii. Uchambuzi zaidi unapendekeza kwamba kuna kisababishi cha mawazo mawili ndani ya taasisi jamii katika kundi hili. Kuna kundi moja ambalo linasisitiza usalama, haki,sheria,ushiriki,na uvumilivu, na kundi lingine la pili la taasisi ambalo hukazania miundo ambayo huhakikisha matokeo sawa na kwamba soko lifanye kazi kwa wote. La kwanza kwa haya makundi huonekana zaidi kupendelea katika sababu za kijamii na la pili sababu za kiuchumi.[8]

Ruzuku ndogo ndogo kama nyenzo ya maendeleo

Ruzuku ndogo ndogo zilikuwa njia moja ambayo taasisi jamii zingeweza kuleta mwonekano wa wazi kwa mashirika yasiyokuwa ya kiserikali na makundi mengine ya kijamii baina ya biashara na sekta ya mashirika kwa njia ya wazi na uwazi. Ruzuku mara nyingi huenda sambamba na shughuli nyingine mbalimbali,ikiwa ni pamoja na kujenga uwezo,kuimarisha uongozi wa jamii n.k – na zilikuwa tu namna ya mwisho kuliko mwisho kwa.wenyewe.

Mengi ya mashirika yalikuwa tu na kiasi kidogo cha akiba kwa ajili ya kutoa ruzuku na kwa hiyo ruzuku zao zilikuwa zinafanana udogo. Kwa kuchukua kiwango cha ruzuku mbalimbali kutoka ndogo hadi kubwa,cha kati kilikuwa kutoka $350 hadi $ 2,500. Pasentali 25 ilikuwa kutoka $110 hadi 1,000 na pasentali 75 kutoka $700 hadi $12,850.

Hata hivyo, hii haikuwa muhimu ni hasara. Mengi ya makundi madogo ambayo taasisi jamii ilikuwa inasaidia ilikuwa haikuwahi kupokea mfuko wa ruzuku kabla na ingehangaika kuchukua kiasi kikubwa. Hatua ya kuomba na kusimamia ruzuku ndogo ilikuwa yenyewe ni ya kimaendeleo kwa mashirika mengi ya jamii. Hata kama gharama za ubadilishaji zilikuwa juu zaidi na ruzuku ndogo ziliweza kuonekana kama uwekekezaji – wa muda mrefu. Mtoa majibu mmoja alifafanua jinsi ruzuku yao ndogo ilivyokuwa

imeleta vikundi vingi visivyo rasmi na fursa za kuhalalisha shughuli zao hadi hatua ambayo waliweza tena kupata ruzuku wao wenyewe moja kwa moja bila taasisi jamii. Wengine walikazania matukio ya uwezeshaji ambayo ruzuku ndogo nayo ingeweza kuwa katika kujenga umiliki wa ndani wa miradi, pamoja na umuhimu wa ruzuku zisizokuwa na masharti:katika maneno ya mtoa majibu mmoja 'Ni tu baada ya kupata ruzuku ndipo hupanga nini wanataka kufanya'.

Hali kadhalika, matumizi ya ruzuku ndogo zenye mahitaji rahisi na kuwezekana kutoa taarifa, kando ya misaada mbalimbali ya kujenga uwezo, pia ilimaanisha iliwezekana kustawi sambamba zaidi, ngazi chache,uhusiano na washirika wa ruzuku ambao waliegemea cha zaidi kuliko fedha pekee. Mtoa majibu mmoja aliona ufikiwaji na ukaribu wa shirika lao kwa vikundi walivyosaidia kama sehemu muhimu ya utambulisho wao: hawakuwa wahisani 'wa kuogopwa'. Ruzuku ndogo pia ilitumika kama mkakati wa kufaa wa kuunganisha kile kilichokuwa mara nyingi kitenganishi kati ya watu na zaidi kushirikisha aina za maendeleo. Watoa majibu wengi walifafanua namna miradi mikubwa ya aina hii kawaida ilivyotekelezwa na ngazi zingine za juu za kitaalam za mashirika yasiyo ya kiserikali mara nyingi ikionekana jambo la kuwazika na la mbali kwa wenyeji.

Utoaji wa fedha na uchangishaji fedha

Ingawa kwa ujumla vyanzo vya utoaji fedha katika kundi hili la mashirika yalitofautiana kwa ukubwa wa umuhimu, wote walihusishwa kuendeleza msingi wa mfadhili wa ndani kwa baadhi ya ngazi. Katika upande mmoja wa ukanda yalikuwa ni mkusanyiko wa mashirika yaliyojiendesha kitaalam, yaliyoanzishwa na bado kupewa fedha na wafadhili wa kimataifa, ambao walikuwa wanatafuta kuunda jimbo la ndani la mfadhili kama mkakati kuhakikisha uendelevu wake wa muda mrefu wa kifedha (hasa pale ambapo wafadhili tayari wanajadili mikakati ya kutoka) na kuongeza umiliki wa wenyeji kwa pamoja. Kwa upande mwingine, hizo zilikuwa ari zaidi za watu wa kawaida, zilizoanzishwa mahususi kwa michango ya ndani (na ambao Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii ulikuwa wa kwanza na mtoa fedha pekee), ambayo ilielekea kuendeshwa bila kuwa rasmi na ambayo ilipambana na changamoto za mizania ya mahitaji muhimu na raslimali finyu. Nyingi ya taasisi jamii zinaangukia katika kundi la 'kati' likiwa linayo mafanikio katika kuvutia michanganyiko ya misaada yote ya ndani na kimataifa.

Jedwali lifuatalo linaonyesha umuhimu wa aina tofauti ya misaada ya fedha. Linatambua mataifa, taifa au serikali za mitaa,sekta za watu binafsi na vyanzo vingine na kufananisha hizi na sehemu ya bajeti iliyofikiwa na kila aina ya utoaji fedha katika mashirika 39 ya utafiti huu.

Sehemu ya bajeti iliyopatikana kutoka aina mbalimbali za utoaji fedha

Chanzo cha fedha	*Hakuna*	*1% hadi 24%*	*25% hadi 49%*	*50% hadi 74%*	*75% au zaidi*	*Total*
Mataifa	8	6	11	6	8	39
Taifa au serikali za mitaa	18	15	0	4	2	39
Shirika	10	18	7	2	2	39
Watu binafsi	5	28	3	2	1	39
Wengine	21	14	1	3	0	39

Zingatia: namba katika jedwali ni namba za mashrika yanayoanguka katika kundi. Na = 39

Bila kujali ukubwa au hali, mashirika yalipata changamoto nyingi za namna moja ilipokuja kwenye kuchangisha fedha kienyeji. Sababu moja kwa hili ilikuwa ni ugeni wa dhana ya taasisi jamii, vyote katika matamani na shughuli zake. Katika njia moja ambayo utengenezaji wa ruzuku mara zote haukuanzishwa kama vitendo vya kawaida, taasisi jamii ambazo zilikuwa zinatafuta kujenga mafungu ya kumiliki pia zilipata ugumu kuelezea dhana. Umiliki unaweza kuhakikisha uendelevu na uhuru wa muda mrefu wa mfuko wa taasisi jamii, raslimali ambayo inaweza kuchukuliwa katika mwitikio wa mahitaji ya jamii. Hata hivyo, kushawishi wafadhili wa ndani kuchangia kwenye mifuko ya kumiliki,wapi mchango ungewekezwa, na asilimia ndogo tu ambayo ingepatikana katika riba ingetumika, lilikuwa ni jukumu gumu kwa wengi. Kama mtoa majibu mmoja kutoka Kusini mwa Afrika alivyoliweka, jibu la watu mara kwa mara lilikuwa moja ya: 'Kwa nini kukuza umiliki wa fedha, wakati kuna umaskini leo?'

Chache kidogo zaidi ya nusu ya mashirika yalikuwa yameanzisha umiliki (22 ya 49). Ukubwa wa umiliki ulielekea kuwa mdogo. Wa kati ulikuwa $32,500, tofauti ya intakwatali ilikuwa kati ya $13,750 hadi 107,000, na kubwa ilikuwa $927,000.

Yaliyopita ya nchi pia yalisaidia kuumba hali ya sasa na dhana kuelekea hisani ya ndani na uchangiaji wa fedha. Kwa mfano,wazo la hisani iliyopangwa kama nafasi kwa vitendo binafsi ilikuwa vigumu hasa kufundisha katika mazingira yenye historia ya utegemezi kwenye nchi au kwenye misaada ya maendeleo ya kimataifa kama chanzo muhimu cha msingi kutoa. Mkurugenzi wa taasisi jamii changa katika Afrika ya Mashariki alifafanua namna, ingawa wajumbe wa jamii walizoea kuchangia kwa matukio maalum kama harusi na mazishi,wakati walipoulizwa kuchangia kwa suala kwa mtoto anayeishi katika mazingira magumu,watu waliliona hili kama jukumu la serikali. Mwingine alitaja changamoto ya kubadilisha tabia katika mazingira yake ya ndani ambapo palikuwa na utegemezi mzito msaada wa kigeni, ambapo jamii ilishakuwa 'zoefu kujifikiria wenyewe kama wapokeaji, kutoa thamani ndogo kwa raslimali zao wenyewe'. Hata hivyo, historia, desturi na dini pia zilitoa zaidi uzoefu chanya wa hisani, ambapo mifuko mingi ya taasisi jamii ilijaribu kuchukulia hapo au kufufua katika jitihada zao za kuendeleza misaada ya ndani. Katika Kusini-Mashariki mwa Asia, kwa mfano, taasisi jamii moja iliyojitokeza ilifafanua jinsi 'watu watakavyojitolea kama sehemu kusaidia watu wengine lakini pia kwa sababu wanapokea 'wema' katika falsafa ya kibudisti'.

Suala la kuamini –au kutoamini –kilikuwa kikwazo kingine kikubwa kujenga jimbo la ndani la ufadhili. Katika jaribio lao la kuchangisha fedha za ndani, taasisi jamii nyingi

mwanzoni zilijaribu kushinda wasiwasi kama kusudio lao. Tena, uzoefu uliopita wa hisani iliyopangiliwa katika nchi zilizopita za Kikomunisti mara kwa mara zilipelekea umma kuwa na wasiwasi mkubwa kama msukumo mpya nyuma yake wa kujaribu kufanya ifanye kazi tena. Hali kadhalika, katika hali ambapo rushwa ilikuwa juu, mara zote kulikuwa na suala muhimu kuliko yote la kutoamini taasisi za namna zote kwa kutokuwa na – uwazi, kusaidiana wenyewe na kutokuwa wazi katika manyanyaso.

Bila mshangao labda, kwa kuwepo na upungufu wa ufahamu na wazo la hisani ya kitaasisi,wafadhili wengi muhimu wa ndani-kama walikuwa wanaelekea kutoa kwa vyovyote – hupendelea kutoa visababisho moja kwa moja kuliko zaidi kupitia walichochukulia kama upatanishi wa gharama. Kama taasisi jamii moja ya Ulaya Mashariki ilielezea 'watu hawaelewi mahitaji ya taasisi za kitaalam na hudharau kutoa gharama za utawala.' Katika hali nyingi, taasisi jamii walijikuta wenyewe katika hali ambayo huwezi kufanya jambo la pili mpaka umefanya la kwanza. Ilikuwa vigumu kuchangisha fedha kwa ajili ya kutoa ruzuku kwa sababu wafadhili muhimu walitaka kujua kikamilifu wapi fedha zao zilikuwa zinaenda na bado bila mifuko hii taasisi jamii zilikuwa na matatizo mengi na upungufu wa fedha kutengeneza aina za ruzuku kwa ukamilifu,miradi ya jamii ya kuonekana ambayo ingeweza kuonyesha kufaa kwa mbinu. Kama mashirika'ngazi ya pili'(yaani hatua moja iliondolewa kutoka wadau wa moja kwa moja wa mradi) ilikuwa pia wakati mwingine vigumu kuhusishwa moja kwa moja na mafanikio ya mradi wowote. Hata hivyo,wengi walielewa kwamba ingechukua muda kujenga aina ya mahusiano ya uaminifu ambayo ingeweza kupelekea kukua kwa aina za wafadhili na ilijenga mikakati ya mpito ikilenga kuunganisha umbali kati ya malengo-kama kwanza kufanya watu washiriki katika shughuli za taasisi jamii, kwa changia muda wao kama watu wa kujitolea,au pengine kuwasilisha miradi iliyochaguliwa awali kwa wafadhili muhimu. Wengine waliliona kiahisi kama swala la ujenzi wa uelewa polepole na imani katika jamii na la kuongoza kwa mifano. Mkurugenzi mmoja wa taasisi alifafanua jinsi yeye mwenyewe alivyofanya kazi kama mtu wa kujitolea kwa miaka miwili ya kwanza na hii ilisaidia kushawishi watu kwamba kusudio lake halikuwa kudhania. Katika maneno ya mwingine: 'watu wanahitaji msukumo kuanza kubadilisha tabia . . . Uaminifu ni muhimu sana: Unaweza tu kuja kama utafanya ulichoahidi kufanya.'

Kwa hizo taasisi jamii zilizofanya na makundi madogo, kulikuwa mara kwa mara na changamoto fulani zilizoambatana na kuchangisha fedha za ndani kutoka jamii pana.

Katika Ulaya Mashariki na Kati,kwa mfano,suala la Roma lilikuwa moja ambalo lilikuwa vigumu kuvutia pesa za ndani; 'suala gumu' lingine lilikuwa hilo la uhamiaji haramu; katika maeneo mengine, taasisi jamii zilizofanya na jamii 'zisizoonekana' (hasa jamii za asili) walikutana na changamoto sawa ilipokuja kwenye kuwakabili wafadhili wa ndani. Katika hali kama hizi, taasisi jamii mara kwa mara zilitegemea kwenye uwepo wa mifuko ya kimataifa-na wakati mwingine ya jumuiya za watu wanaoishi nje – ili kuweza kuzungumzia suala kote.

Kwa taasisi jamii nyingi,uwezekano mkubwa wa aina ya msaaada wa awali ilikuwa kutoka biashara ya ndani,kama wangeweza kushawishika na thamani ya kufanya na taasisi jamii kama njia ya kuwapunguzia adha ya utawala na ya mfuko wao kutumiwa kwa mafanikio zaidi. Ingawa kuvutia michango kutoka watu binafsi ilikuwa changamoto kwa mazingira mengii, wengi wa waliohojiwa walikazia umuhimu aina hii ya msaada katika kuhakikisha umiliki wa kweli wa jamii wa taasissi. Mtoa majibu mmoja alifafanua jinsi hisani ya umma haitakiwi kuchukuliwa kama 'duka la mitindo' la 'mapambo ya vito la kikundi kidogo cha watu wenye nguvu zaidi na faida kuliko wengine' lakini isipokuwa ni 'bidhaa ya mlaji . . . inayopatikana katika duka la vyakula'.

Hitimisho

Utafiti wetu unapendekeza mistari mingi ya kutumainiwa kwa maulizo zaidi na maendeleo. Tunatamka haya hapa kama kihusishi kwa majaribio zaidi.

1 Taasisi jamii yaweza kuwa ni sehemu inayokosekana katika mambo tata ya maendeleo ya kimataifa. Kuna mjadala unaokua juu ya msaada unaofikia sehemu za jamii ambako imelengwa. Fedha kutoka wakala wa kimataifa hudakwa na makundi ya watu walionacho, kiasi kwamba fedha hushindwa kufikia watu wa chini. Taasisi jamii hutoa mbinu ya kufikia wote wenye kuhitaji zaidi, wakati wanapotoa uongozi wa ndani,umiliki na uwajibikaji.

2 Taasisi jamii hujenga 'uaminifu' kama moja ya majukumu yake ya kwanza. Hiki ni kipengele muhimu katika kuzungumzia umaskini. Watu wanaojiona kutengwa kutoka wengine na kutoaminika au taasisi yao haitawezekana kuweza kupambana na umaskini katika jamii zao. Kuna ongezeko la uelewa wa jukumu la tabia na mwenendo katika jamii, kuona wazo la 'mwonekano wa nje wa jamii' kama sura muhimu katika maendeleo yenye mafanikio.

3 Kuna thamani ya pekee katika fedha za ndani. Hata kama kiasi ni kidogo,ni muhimu kwamba wenyeji wanachangia rasilimali zao wenyewe kwa ufumbuzi wa matatizo yao. Maendeleo ya jamii ni juu ya zaidi ya fedha na bado kiasi kidogo cha fedha kwa kiasi kikubwa kina thamani.

4 Mwisho, kwa kutengeneza ruzuku ndogo ndogo na kujenga mahusiano na mashirika ya chini,taasisi jamii inaweza kuchukua jukumu la kuwezesha sauti za wenyeji,wakiwemo maskini, kusikika. Ingawa wengi wa taasisi jamii katika kundi hili hawapendi lugha ya 'haki jamii', uimara wao wa tamaa yao ilikuwa kuwezesha 'watu binafsi na vikundi kuwa na nguvu ya kuwa na sauti katika masuala ambayo yanayowagusa wao'.

Nini kingine

Tuko na ufahamu kwamba hiki ni kipande kidogo cha kazi na chenye mipaka. Tunapanga kuendeleza utafiti huu kwa kuzamisha uelewa wetu wa kundi la wasaidiwaji wa sasa watavyokuwa wanaendelea mbele,na pia kwa kuongeza makundi mapya kama watakavyokuwa wakijitokeza kwenye utaratibu.

Tunategemea pia kujumuisha watu katika majadiliano na kukukaribisha wewe kupeleka maoni katika makala hii kwa Jenny Hodgson katika jenny@globalfundcf.org.

Marejeo

1 Uchambuzi wa mwenendo kwa kuegemea katika alama za takwimu tano zilizoripotiwa katika hali ya kidunia ya taasisi jamii. Taarifa kutoka 2000–08 (www.wingsweb.org).

2 Shirika moja lilikaribishwa kuwasilisha mapendekezo mawili kwa miradi tofauti kwa hiyo jumla ya maombi yalikuwa kwa miradi 50 kutoka mashirika 49.

3 Taasisi jamii ya kwanza nje ya Amerika Kaskazini na Ulaya Magharibi zilizoanzishwa katikati ya mwaka 1990, katika Ulaya Mashariki, Mexico na Afrika Kusini.

4 Uchaguzi wa viashiria ulipatikana kutoka muhtasari wa tathmini ya kazi ya Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii (2006–08).Viashiria vilichaguliwa kutoka vyanzo mbalimbali ikiwa ni pamoja na fasihi kwenye mtaji jamii na tathmini ya Benki ya Dunia ya miradi ya maendeleo. Kulikuwa na aina kuu tatu za viashiria vilivyochaguliwa, kila kimoja kikifanana na moja ya lengo la Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii. Aina ya kwanza ya kiashiria kilipima athari katika maeneo fulani. Cha pili kilipima ujenzi wa eneo la hisani jamii katika Ukanda au Kiulimwengu. Cha tatu kilipima athari katika sera na vitendo watengeneza sera na wenye rasilimali.

5 Katika mwaka 2007, Kikosi Kazi katika Hisani kwenye Haki Jamii na Usalama kiliitishwa na Christopher Harris, ambaye wakati huo alikuwa Afisa Mwandamizi wa programu ya watu wenye shida katika Taasisi ya Ford, kuendeleza fikra na kujenga maelewano ya pamoja juu ya maana ya hisani kwenye haki jamii na usalama, kutambua (upya au zilizopo) nyenzo kutathmini kwa mafaniko makubwa athari za kazi yetu,na kupanua zaidi mtandao wa watu binafsi wanaopendelea kuona ongezeko la taasisi za hisani na kuimarisha msaada wake kwa kazi ambazo huendeleza mabadiliko ya muundo wa haki. Ona http://p-sj.org/node/68.

6 Ruesga, G.A. and Puntenney, D. (Machi 2010). Hisani Haki Jamii: Mfumo wa Awali kwa Kuweka Kazi hii.Kikundi Kazi cha Hisani kwa Haki Jamii na Usalama

7 Alfa ya Chronbach = 0.73

8 Matokeo haya yalitokana kwenye uchambuzi wa vipengele vikuu kwa kutumia kigawo cha mzunguko cha varimax. Licha ya namba ndogo, matokeo yalieleweka na vigawo viwili vilielezea mbili ya tatu ya kuhitilafiana.

Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii

Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii (MDTJ) ni watoaji wa ruzuku kwa watu wa chini wanaofanya kazi kuendeleza na kusaidia Taasisi za jamii za hisani kuzunguka dunia. Hufanya kazi na taasisi jamii binafsi na watoaji ruzuku wengine wa ndani na mitandao yao wakiwa na mtizamo kwenye nchi zenye kipato cha chini na cha kati. Kupitia ruzuku ndogo ndogo, msaada wa kitaalam na kukutanisha MDTJ husaidia hizi taasisi za ndani kuimarika na kukua ili ziweze kutimiza uwezekano wake wa kuwa nyenzo ya maendeleo ya ndani ambayo huongozwa-na jamii.

Katika kutengeneza kielelezo chake cha utoaji wa ruzuku, Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii imechanganya tathmini na mfumo wake wa utawala,ili kwamba taratibu zote zinazotumika katika kutoa ruzuku zitoe takwimu za tathmini. MDTJ inapenda kutambua msaada wa wafadhili wafutao katika mwaka 2009–10 ambao bila wao taarifa hii-na kazi iliyo nyuma yake-isingewezekana:

Taasisi ya Ford
Taasisi ya Charles Stewart Mott
Taassisi ya W.K Kellog
Mfuko wa ndugu wa Rockefeller
Taasisi ya Mfalme Baudouin

Taasisi ya Dunia ya Mfuko wa Kusaidia Jamii

engo la EISA
Ghorofa ya chini
Barabara ya 14 Park
Richmond
Johannesburg 2092

WWW.globalfundcf.org
info@globalfundcf.org

Nyumba ya Jamii
Park Citylink
Barabara ya Albert
Belfast BT12 4HQ
Ireland Kaskazini

Kampuni yenye uthamini.

Iliyosajiliwa Ireland Kaskazini Na.NI073343

Hisani iliyosajiliwa Namba XT18816

Kifungu cha 21 cha Makampuni (Afrika Kusini): 2010/000806/08

Imechapishwa na Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii.Haki zote zimehifadhiwa

Taarifa hii imechapishwa kwa matunda ya FSC iliyoruhusiwa kutoka vyanzo endelevu

Mfuko wa Dunia wa Taasisi Jamii

www.globalfundcf.org

Juni 2010